APPENDEX "A"

OFISI YA RAISI TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI
SHULE YA SEKONDARI ILOGOMBE,
S. L. P. 464,
MAFINGA.
02.12.2019

JINA LA MWANAFUNZI_____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILOGOMBE WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2021

1 UTANGULIZI

Nina furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari **ILOGOMBE** ipo umbali wa Km110 kutoka Halmashauri ya MUFINDI, kata ya KIBENGU, Kijiji cha Ilogombe. Usafiri wa basi kutoka Mafinga unapatikana katika kituo cha mabasi cha mafinga, Nauli ni Tshs.8,000/=. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ***11/01/2021*** **.** Fika shuleni saa 1:00 kamili ukia na vifaa vyote vya kujifunzia ulivyoagizwa.

2 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 **SARE ZA SHULE.**

a) Sare ya shule hii ni kama inavyoelekezwa katika jedwali hapo chini.

WAVULANA	WASICHANA
Suruali mbili pana rangi nyeusi	Sketi(Rinda box) mbili rangi nyeusi
Shati mbili nyeupe mikono mifupi	Shati mbili nyeupe mikono mifupi
Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba.	Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba.
Tai mbili rangi nyeusi	Tai mbili rangi nyeusi
Sweta la kufuma V- shape rangi ya bluu	Sweta la kufumaV-shape rangi ya bluu

b) Sare ya michezo kwa shule wavulana bukta ndefu na tisheti rangi yeyote, kwa wasichana track suit rangi yeyote.

2.2 VITU MUHIMU.

Mwanafunzi aje na:

i. Daftari kubwa kumi, kalamu na mkebe wa hesabu.
ii. Jembe moja na mpini wake pamoja na fyekeo/kwanja moja.
iii. Kamusi ya kiingereza.
iv. Godoro, blanketi, mto na shuka watavikuta shuleni kwa mchango wa shillingi elfu ishirini(20,000/=) kwa mwaka.
v. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko) kwa ajili ya matumizi yake binafsi hapa shuleni.
vi. Gauni/shamba dress damu ya zee kwa wasichana kwa ajili ya shughuli za shamba.
vii. Ndoo mbili za lita kumi.

3.1 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na OFISI YA RAISI TAMISEMI. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kw aviongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(Preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kutunza mali za umma.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocain, mirungi, kuberi na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza na kushiriki, kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

4 Mambo mengine muhimu.

4.1 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:-

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

…….

PRIVATUS HAULE
MKUU WA SHULE.
SIMU: 0767-178869 AU 0787-178869 AU 0716-103839

APPENDEX "B"

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY,

ILOGOMBE SECONDARY SCHOOL.

MEDICAL EXAMINATION FORM(To be completed by medical officer in respect of all form one entrants)

Pupil's full name ……

Age…… **Years**…… **Sex**……..

Blood count (Red and White)……

Stool Examination……..

Syphilis and other venereal Diseases Test…….

……
……..

T.B. TEST…….

Eye Test……..

Ears……..

Spleen……..

Abdomen……..

Urine for Plamotest…….

Test of pregnancy(For girls only)……

ADDITIONAL INFORMATION:

(If any) e.g physical defects impartment)

Infection chronic or family diseases etc……

I certify that the above pupil is Fit/Unfit to pursue his/her Lessons/Duties as required.

Station…… **Signature**……

Date…….. **Designation**……..

Note**: MEDICAL OFFICER**:

At the time of Examination please treat the individual for any ailments you note.

Pupils/employee. This complete form should be sent to the school with your acceptance form bought when you come to school. No pupils and enroll person, any employee with certification or physical fitness.

KIAMBATANISHO "C"

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

SHULE YA SEKONDARI ILOGOMBE,

S. . P 464

MAFINGA- IRINGA.

JINA LA MWANAFUNZI……

1. Jina kamili……

   Tarehe ya kuzaliwa…….. mwezi……. Mwaka…….
2. Kabila……. Taifa……
3. Dini na Dhehebu……..
4. Jina la Baba…….
5. Anwani ya mzazi/mlezi……..

   ……

   Namba za simu……
6. Kazi ya Baba/Mlezi……
7. Jina la Mama…….. Kazi yake……..
8. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana…….
9. Jina na Anwani ya Mlezi wako(kama si Mzazi)……..

   ……

   Namba ya simu……..
10. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi(taja sehemu moja tu utakayo kwenda kila wakati)

    ……..
11. Nathibitisha kwamba taarifa zote nilizotoa ni kweli na sahihi.

    Sahihi ya Mzazi/Mlezi……. Tarehe……

    Sahihi ya Mwanafunzi……. Tarehe……..